# KICHAPO CHA KARAHA na Humphrey Onkoba

*Onkoba Humphrey* ni mzawa wa kaunti ya Nakuru. Ni mwandishi mwenye tajiriba ya ufundishaji wa lugha ya Kiswahili. Amefunza katika shule tofauti nchini. Kwa sasa ni mwalimu wa *shule ya upili ya Karati* kaunti ya Nyandarua. Onkoba ni mtahini wa kitaifa katika somo la fasihi. Ameandika hadithi kwenye diwani ya *Nguvu za Sindano na Hadithi Nyingine.*

Mpata na Mpatanishi waliishi maisha ya raha mustarehe. Hawa walikuwa "ndugu" wa toka nitoke. Waliishi katika kitongoji cha Bondeni. Kijijini humo mlisheheni mabonde yaliyogeuka kuwa kero katika msimu wa mvua. Adha za Bondeni zilitokana na utelezi wa mara kwa mara ambao haungewaruhusu waja kusafiri kutoka janibu moja hadi nyingine. Mpata na Mpatanishi walisalia kiamboni mwao wakiwachunga kondoo wa ajuza mmoja aliyekuwa ametia fora maadamu alikuwa mkwasi mwenye ukwasi wa kuliliwa ngoa na adinasi wenye hulka za kulaza damu gangeni. Kondoo wa ajuza huyo walikuwa wa kisasa wenye manyoya mazito mazito yaliyowaauni kustahimili baridi shadidi iliyozizima kwenye msimu wa kipupwe. Mpata alizoea kumtaarifu Mpatanishi kuhusu taarifa zozote zilizotukia mle Bondeni. Leo hii mbiu ya mgambo ililia na bila shaka jambo au mambo hayangekosa kujiri. Mpata alifika hima kitendeni na kumpata Mpatanishi angali anaforota kitandani huku amejifunika gubigubi kwa blanketi lake kuukuu. Blanketi hili lilikuwa limenunuliwa na abu yake alipokuwa akitoka kwenye safari ya nchi ya Zambarau. Blanketi hilo lilikuwa teketeke limeundwa kwa usufi ambao ulikuwa umechanika chanika kutokana na mpito wa wakati.

"Leo ni leo asemaye kesho ni mwongo," alianza Mpata. Naye Mpatanishi akauliza, "kulikoni ndugu yangu? Kwema kweli?" aliakamatwa na wahaka "Kwema hakujawa ila wema wenyewe umeadimika humu mithili ya…" Akimkatiza, Mpatanishi alijibu, "ya mizizi yam awe au maziwa ya kuku?" "Yote ni mamoja. Sioni tofauti kwayo!" Mpata alijaribu kumsimanga Mpatanishi. "Haya! Ebo! Iweje basi huna furaha riboribo kakangu?" Mpatanishi alimdahili Mpata.

“Dunia mwendo wa ngisi kweli,” Mpata alimwaga lulu. “Yule ngisi mmoja wa majini au yupi?” Mpatanishi alidakia.
“Naam, bila shaka ni yuyo huyo!” Mpata akakazania.

Hapo ndipo Mpata na Mpatanishi walipoamua kumwagiana dukuduku za aushini mwao. Waliliwazana na kupigana pambaja kama wanawakiwa. Kumbatio hilo nusura liwatoneshe machozi. Kumbato hilo lilikuwa la miaka na mikaka kwani halijawahi kushuhudiwa kati yao. Mpata alimpasulia mbarika Mpatanishi na kumweleza kinaganaga kwamba jirani yao wa miaka na dahari alikuwa akimsingizia kosa la ubakaji. Jirani huyo alidai Mpata alimtia doa bintiye wa miaka kumi na mitano katika jumba lao la kifahari siku ya karamu ya kusherehekea kuzaliwa kwa mnuna wake. Lo! Hilo lilimtetemesha Mpatanishi ja kuku aliyekunywa maji ya msalani. Akamaka na kushika tama huku macho yake yamemtoka pima. Hakujua ajibu vipi shtaka hilo ilhali hizo ndizo zilikuwa hulka za Mpata.Tabia zake za kuwamezea mate vidosho wa wenyewe ambao hata hawakuwa wamekaribia kuvunja ungo. Hili la ubakaji lilikuwa limepita mipaka. Shutuma mbovu.

Si mara moja wala si mara mbili Mpatanishi alikuwa amejitolea sabili kumkanya na kumshauri Mpata dhidi ya kuchuna ngozi na magashi wa umri mdogo mno. Huenda akajitia matatani, ila hayo yote yaliangukia masikio yaliyokuwa yametiwa nta. Mpata hakusikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Aligeuka sikio la kufa ambalo kwa ukawaida huwa halisikii dawa. Mpatanishi aliachama tu asijue la kutenda, kwani ni vipi angemwauni nduguye kutokana na mwiba huo wa kujidunga? Mpatanishi aliwaza na kuwazua mpaka akafikia uamuzi wa kipekee. Uamuzi wenyewe ulikuwa wa kumwendea mzee Tambolo na mkewe ili kuwadadisi kuhusu ukweli wa mambo. Pengine ni kisingizio tu kilichoelekezewa sahibu wake wa tangu azali. Japo Mpata alikuwa na walakini katika maisha yake, huenda akaponea chupuchupu, pengine ataponea tundu la sindano itakapogundulikana kuwa hizo zilikuwa tetesi tu kutoka kwa jirani yake.

Mpatanishi alifunga mwendo guu mosi guu pili, hadi alikostakimu mzee Tambolo. Alipobisha hodi tu alilakiwa na sauti nyororo ya kike. Huyu lazima ndiye bintiye mtuhumiwa wa kutiwa doa na Mpata. Mpatanishi alijiambia kimoyomoyo. Makaribisho aliyopewa yalikuwa ya staha. Akaingia ndani ya sebule na kujipwetereka kochini. Wenyeji wake walijitokeza; mtu na mkewe. Wajihini mwao ishara za kuhamaki

zikijianika waziwazi. Mpatanishi alikuwa kweli kajileta kwenye domo la bafe kujaribu kuleta upatanishi kati ya makundi mawili hasimu. Aliyekuli kuwa msema kesho ni mwongo hakughilibu katu. Mpatanishi alikuwa ashaambulia leo yake. Leo ni leo.

“Umefanya vyema kufika huku kwetu Mpatanishi,” Mzee Tambolo alikata kalima na kuendelea, “Ila umechelewa mno, tayari tumeshastaftahi. Hatuna salio lolote wala masazo ya kupa. Hebu tuelezee, la mno?” Mpatanishi aliingiwa na wahka, kijasho chembamba kilijipenyeza kipajini mwake, akaanza kutweta kwa pumzi za juu. Akaona kisunzi nusura aanguke sakafuni pu! Nakwambia hapo angetoka na jeraha la mwaka madhali sakafu yenyewe ilikuwa imesakafiwa na taili nyeupe pe! Ila Mpatanishi alijizuia kugota sakafuni kwa kujiegemeza kwenye nguzo moja imara iliyosimama jadidi katikati ya baraza na sebule lao. Kiwi kilimvamia machoni huku akisepetuka kushoto tena kulia. Alijaribu kuyafikicha maozi yake ili angalau aweze kuona barabara. Licha ya juhudi zote hizo hakufanikiwa kurejelea hali yake ya kawaida. Alijipata akipiga magoti kwenye zulia jekundu ja ngeu. Alianza kujutia mjo wake humo. Mzee Tambolo na mkewe walimtilia pondo aketi kwenye kiti cha kukunja, kilichokuwa kimeundwa kwa makuti. Mpatanishi alijikaza kishujaa kuinuka kutoka kwenye jamvi hilo. Lahaula! Alishindwa! Woga ulizidi kumvaa huku maswali yakimcharura akilini mwake. Mbona alijileta kwenye domo la simba? Mpatanishi alijipata akilala kifudifudi sakafuni tena maadamu kiti kile cha kukunja kilikuwa kikuukuu. Hakikuweza kustahimili uzito wake Mpatanishi, kilisikika kikilalama kwa sauti za huruma. Kicheko kikubwa mithili ya radi kilisikika kikihanikiza hewani. Anga yote humo ndani ilitwaliwa na vicheko vya kubeza kutoka kwa mkewe Tambolo. Haya yalikuwa kama mauzauza aushini mwa Mpatanishi kusema kweli hajawahi kufikwa na yaliyomfika siku hiyo.

“Kama umejia ya Mpata huku basi huna lako!” Sauti laini ya mkewe Tambolo ilipasua ukimya uliojiri baada ya kicheko chake cha aiskrimu.

Mpatanishi alikumbatiwa papatu na tumbojoto. Kudhani kuja kwake kumpatanisha mwenzi wake kulisalia tu dhana isiyo na mashiko yoyote. “Kila siku madhila yakiwafika waja wewe ndiwe hujiona mpatanishi mkuu. Leo hii utawezana na suala la kuchusha la mwenzio mpata?” Mzee Tambolo alipasua mbarika.

“Simile baba! Mwenzio unayemsema anaviuma vidole vyake nusura avikate kwa tendo lenyewe, msameheni.” Mpatanishi alikiri kwa niaba ya Mpata. “Fyata huo uli… uli… ulimi wako! Hu…hu…huna ha…ta izara weye!” Mzee Tambolo alimkaripia Mpatanishi kwa kigugumizi chake.

Hadi hapo Mpatanishi alinywea na kugwaya ajabu. Aliingiwa na ububu kwani alimaizi fika moto ulikuwa umewaka kama uliochochewa kwa wimbombo na kungeteketea wakati wowote. Endapo angeendelea kuzungumza. Alijishika tama na kusononeka ajabu. Alijutia sana kilichomtuma kufika humo. Alijutia sana ujuaji wake wa kujifanya kujua siku zote. Alijutia sana moyo wakewa upatanishi. Alijuta, akajuta hata zaidi ya zai…. Aliona hata picha zilizokuwa zimetundikwa kutani mle sebuleni zikimchekelea kwa! Kwa! Kwa! Kalenda nazo ziliongeza dhihaka kwa kumkodolea macho kodokodo kana kwamba zilishuhudia filamu ya bure bilashi. Mpatanishi aliemewa akabaki kuachama tu. Bi. Tambolo naye hakumeza mate, alitema maneno mfululizo. “Wee, Mpatanishi unaweza kuhisi vipi kilaika chako kikibakwa? Hujui utungu wa mwana kwa kuwa huna kikembe chochote! Vipi uje hapa kusema Mpata ajuta ilhali mwenyewe ajitanua kifua mjini jinsi hawezwi na yeyote wala sheria?” Bi. Tambolo alifoka. “Mpata lazima ale kalenda! La sivyo ahamie kijiji kingine kule mkono wa sheria hautamfikia.”

Naya Mzee Tambolo alishinikiza. Ujio wa Mpatanishi haukuchangamkiwa kweli na wenyeji wake. Ilidhihirika dhahiri shahiri kuwa hakukuwa na mlahaka aali kati yao. Mpatanishi aliomba idhini ya kumhoji Tiara bintiye Tambolo, mtuhumiwa wa ubakaji. Tiara ndiye aliyekuwa amemfungulia Mpatanishi mlango alipoubisha ila la kushangaza ni kwamba Tiara mwenyewe hakuonyesha dalili zozote za kubakwa. Alikuwa mzima kama kigongo. Kutembea kwake hakukuwa na taksiri yoyote. Mpatanishi alijiwazia kimoyo moyo. Yeyote aliyebakwa huwa na shida ya kutembea aghalabu. Tiara alikuwa anapiga misamba kama ibada. Bila maumivu wala kuchechemea kwokwote kulijidhihirisha. Hali hiyo ndiyo iliyomfanya Mpatanishi aingiwe na shaka na kuona hapa ni kama kuna kuchezewa shere kunachezwa na kina Tambolo. Aidha, kuboboja kwingi maneno kutoka kwa aila hiyo kulimchochea Mpatanishi kudhania kuna jambo fiche. Dalili za mvua hizo na bila shaka huwa mawingu. Mawingu meusi ti!

Sala la kumdahili Tiara lilitupiliwa mbali kama taka. Mzee Tambolo alijinaki kwamba yakishamwagika hayawezi kuzoleka. Bi. Tambolo naye akamshurutisha Mpatanishi alizike wazo hilo katika kaburi la kina kirefu ajabu! Mpatanishi aliridhia bali shingo upande. Vizingiti ni vingi vilivyokuwa vimeezekwa. Mpatanishi alianza kushawishika nafsini mwake kuwa Mpata alikuwa amelimbikiziwa madai ya uongo. Hiki kilikuwa kisa cha kikulacho ki nguoni mwako. Anayeliwa ni Mpata na hawa aliodhani walikuwa majirani wema kutoka zamani. Majirani aliowatumikia kwa moyo mweupe sawa na pamba enzi zile walizomhitaji sana.

Kimya kilikuwa kimetawala ukumbizoni hata chungu wangepita hayo nyayo zao zingesikika zikikanyaga hatua baada ya hatua sakafuni. Maongezi yalikuwa yamegonga mwamba. Mpatanishi aliamua kufunga kinywa chake, nao wenyeji wake walikuwa wamezungumza hadi wakachoka. Saa za chamcha zilikuwa zimetimia, Bi. Tambolo alitoka nje kwenda kumsaka bintiye Tiara. Hakumpata. Mzee Tambolo naye aliamua kujiunga na mkewe huko nje kumtafuta waridi wao. Walizunguka kila mahali lakini hawakumtia machoni. Kumbe naye Tiara alikuwa tu chumbani mwake akifuatilia matukio hayo kwa umakinifu. Alijitokeza na kuja sebuleni. Kwa bahati nzuri wavyele wake walikuwa wanamsaka huko nje. Hii ilikuwa tijara kwa Mpatanishi. Alimwona Tiara akidondokwa na machozi njia nne nne huku akimjia alikokuwa amekiti. Tiara alifika na kuketi karibu na Mpatanishi. Mpatanishi alimdadisi nini kilichokuwa kinamliza. Tiara aliamua kumwaga mtama bila woga. “Babangu na mamangu walinipa pressure nimsingizie Mpata, “alianza Tiara. “Umsingizie kuhusu nini na kwa nini?” Mpatanishi alitaka kujua. “Eti alinibaka kwa ajili alikataa kuwatumbuiza wageni siku ya sherehe ya Birthday yangu.”

“Salaale! Kwa hivyo ni uongo hukubakwa?” “Naam, Mpata hajawahi hata kunigusa kamwe!” “Pole sana Tiara kwa yaliyokufika. Asante kwa kukiri kwangu.” “ka… ka… kari…kari…bu, sipendi vile wazazi wangu wanavyotaka kumfunga Mpata. Vile vile si haki, ukweli ndio huo sasa.”

“Naam, bila shaka umedhihirisha busara na ukomavu binti mdogo.” “Ndio, Mpatanishi wajua siku zote utatuweka hu…,”

“Huru gani? Tena ukweli upi huo!” Kwa pamoja Mzee Tambolo na mkewe walimkatiza binti yao.

Hawakujua tayari alikuwa ashafichua ukweli kwa Mpatanishi ambaye sasa ameweza kutenga hadaa zao kama giza na mwanga. Mbio zao za sakafuni zimefika ukingoni hatimaye. Ilikuwa zamu ya Mpatanishi kuwabeza na kuwakaripia mahasidi hawa wawili kwa ghadhabu zisizo na ukomo. Aliwazomea kwa ukali wa samba. Aliwaeleza kinaganaga kwamba hila zao zimegonga mwamba. Hila za kumtaka Kumsakama Mpata kwa mafao yao ya kibinafsi. Ama kweli njia ya mwongo huwa fupi siku zote. Njia yam zee Tambolo na mkewe imefupika ajabu. Walidhani wao ni pwagu kumbe leo hii wamepata pwaguzi. Ni vyema kufahamu kwamba siku ya kima kufa miti yote huteleza. Siku ya kina Tambolo na tambo lake pana ilikuwa imebisha hodi. Walijionea soni huku wakiuma kwa mochonge, magego na masagego vidole vyao vya shahada. Walipiga dua kwa Mola safafu ipasuke iwameze ili wafilie mbali japo sala zao hazikuelea hadi mbinguni. Walitafuta pa kufichia nyuso zao wasipate, chambilecho mwungwana akivulia nguo huchutama. Lebasi zao zilikuwa zimevuliwa kwa kuraruliwa raru raru na binti yao mpendwa. Hawakuamini kwamba binti yao waliomuenzi ja mboni ya macho angewasaliti. Walijaribu kumrai Mpatanishi awasamehe lakini rai zao zilikuwa kama kumpigia mbuzi gita. Ziliambulia patupu. Mpatanishi akala yamini kuwa sheria itachukua mkondo wake waama sheria ni msumeno hukata mbele na nyuma. Machozi yalianza kuwalenga wanafiki hawa. Walidhani machozi yangewakinga dhidi ya maovu waliyomtendea Mpata.

Mpatanishi alimpa shukrani jazila Tiara na kumwakikishia ulinzi wa bure ili asidhuriwe na wavyazi wake. Nao Tambolo na mkewe wakashurutishwa kujiandaa mara moja kwenda kumwomba msamaha Mpata kwa kumpatanisha na maovu. Maovu yaliyomchafulia jina lake adhimu, tena adimu kulijenga upya miongoni mwa binadamu wenye damu miilini mwao. Hukumu dhidi ya Tambolo na barafu wake ilitolewa kulingana na mujibu wa sheria za Bondeni. Habari hizo zilipomfikia Mpata, aligubikwa na furaha ghaya. Alijihisi mwepesi kama mbayuwayu. Alijiona mshindi kwani sasa angetulia tuli nafsini mwake. Alipoulizwa wanafiki walewale wafanyiwe nini, Mpata bila kukawia alisema sheria za Bondeni zichukue mkondo wake jinsi maji hufuata mkondo au bendera hufuata upepo. Hivyo ndivyo hatima ya Mzee Tambolo na mkewe ilivyotimia japo walikuwa wakubwa wa tambo, sheria zenye uzito wa nanga hazikuwasaza.

# Jinyakulie nakala hii ili kuzidi kusoma